



No. 3 G Chabruma Street, off Ali Hassan Mwinyi Rd,
Ada Estate, Mbuyuni, Kinondoni Dar es Salaam
P.O. Box 60243, Dar es Salaam TANZANIA

📞 +255-22-2666441
📠 +255-766-430337/655-730337
Email: mariyclinic@ymail.com
Website: www.hmmcltd.com

HEALTH PUBLICATIONS / MAKALA YA AFYA

UZAZI KWA NJIA YA UPASUAJI (CAESAREAN SECTION)

Uzazi kwa njia ya upasuaji ni mojawapo ya njia mbadala ya kujifungua kwa kumtoa mtoto kutoka kwenye kizazi cha mama kuititia ukuta wa tumbo. Wajawazito hujifungua kwa upasuaji endapo kuna tatizo la kiafya linaloweza kuhatarisha maisha ya mama mwenyewew au mtoto, au/na kuzuia uwezekano wa mama kujifungua kwa njia ya kawaida, yaani kuititia ukeni. Takwimu za afya zinaonyesha kuwa, kiwango cha uzazi kwa njia ya upasuaji kinaongezeka duniani kote. Ongezeko hili linatokana na ongezeko la ubora na upatikanaji wa huduma bora za afya ya mama na mtoto wakati wa kujifungua, na pia ongezeko la ubora wa takwimu za huduma ya afya, kwa ujumla. Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania, asilimia kubwa ya vifo vy'a kina mama na watoto wachanga hutokea wakati wa kujifungua na, moja ya visabishi vy'a vifo hivi ni ukosefu wa huduma ya dharua wakati wa kujifungua, mojawapo ikiwa huduma ya uzazi kwa njia ya upasuaji. Hivyo, huduma ya uzazi kwa upasuaji inapaswa kufikika kwa urahisi na kutolewa kwa ubora wa kuwango cha juu ili kuhakikisha matokeo mazuri ya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Huduma ya uzazi kwa upasuaji inaweza kutolewa kwa njia mbili; aidha kwa dharura (Emergency) au kwa kupanga (Elective).

Sababu kuu za kujifungua kwa upasuaji kwa dharura ni kama zifuatazo:

1. Maendeleo yasiyordhisha ya uchungu wa kujifungua (Uchungu pingamizi) kutokana na nyonga nyembamba au mtoto mkubwa au mtoto amelala vibaya au watoto mapacha.
2. Mashaka au uhakika wa tatizo la mtoto, aidha mtoto kuchoka au tatizo la mama linalohatarisha uhai wa mtoto tumboni.
3. Kovu kwenye kizazi kutokana na kujifungua kwa kupasuliwa uzazi uliyopita au matibabu ya kizazi kwa njia ya upasuaji (mf. Kuondoa uvimbe wa kizazi).
4. Kutoka damu nyingi ukeni kutokana na tatizo la kondo la nyuma kuachia kabla ya kujifungua.

Sababu nyingine za kujifungua kwa upasuaji kwa kupanga ni kama zifuatazo:

1. Mtoto kutanguliza makilio au kulala vibaya baada ya wiki 36 za ujauzito.
2. Ujauzito wa mapacha endapo watoto ni wakubwa au wamelala vibaya.
3. Ugonjwa unaohatarisha maisha ya mama endapo atapata uchungu wa kujifungua (ugonjwa wa moyo au mapafu)
4. Historia ya kupasuka msamba daraja la 3 au la 4 katika uzazi uliyopita
5. Historia ya uchungu wa muda mrefu au/na kuzalishwa na vacuum
6. Matokea mabaya katika uzazi uliyo pita mf. Kuzaa mtoto mfu, kuharibika kwa mimba mara kwa mara, n.k.

Uhakika wa mafanikio na matokeo mazuri ya kujifungua kwa upasuaji unategemea uwezo wa hospitali kutoa huduma zingine za dharura kama huduma ya gari la kubebia wagonjwa (Ambulance service) and huduma ya damu (blood transfusion)

Na Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Homoni na Uzazi – Maria Clinic, Dar es Salaam

Kwa Huduma ya Kuonana na Daktari Bingwa piga simu namba:

+255 766 430337/+255 754 587900/+255 755 085586